



The Regional Women's Enterprise Unit



Backing Business in the West Midlands

Karibu Regional Women's Enterprise Unit

Karibu kwenye Shirika la Kijimbo la Midlands Magharibi la Umoja wa Wanawake watendaji (West Midlands Regional Women's Enterprise Unit – RWEU) – lililo zinduliwa mwezi Mei 2006. Lengo la RWEU ni kuongeza idadi ya wanawake watendaji katika jimbo zima.

Madhumuni yetu ni kuwasaidi kutekeleza ndoto zenu, ili kusimama kidete na kuanzisha biashara zenu wenyewe, au kutekeleza mahitaji kwa ajili ya kukuza na kuendeleza biashara mnazo fanya.

Utapata kupewa ushauri na mafunzo na wataalamu bila ya malipo yoyote kuhusiana na jinsi ya kuendesha shughuli za kibiashara kupitia Shirika la Wanawake la Maendeleo ya Kibiashara (Women's Business Development Agency – WBDA) au Shirika la Wanawake watendaji Vijijini (Women in Rural Enterprise – WIRE), walio washirika katika maendeleo na uvumbuzi RWEU.

Huduma hii haitegemei ujuzi, hali yako ya kifedha au elimu, umri, kabila, uwezo au ulemavu – mradi tu unataka kuanzisha na kuendeleza biashara yako... tupo hapa kukusaidia.

Shirika la RWEU linadhaminiwa kifedha na Shirika la Maendeleo ya Kijimbo la (Advantage West Midlands), Dti's Shirika linalo husika na biashara ndogo-ndogo (Dti's Small Business Service) na Shirika la Huduma kwa jamii la Ulaya (European Social Fund).

Tuna toa huduma gani

Je, wewe ni mwanamke unaye fikiria kuanzisha biashara yako, lakini haujui pakuanzia?

Labda pengine umesha anzisha biashara yako na unahitaji biashara hiyo ipige hatua nyingine, au pengine unahitaji ushauri kuhusiana na kuajiri na kuongoza wafanyikazi?

Kwa mahitaji yoyote yale ya biashara yako, tunatoa huduma bure ili kuwaunga mkono wanawake wanao fikiria kuanzisha, au walio tayari na shughuli zao za kibiashara ikiwa ni pamoja na huduma kama:

- Kujenga ustadi na kuzalisha mawazo ya kibiashara
- Kupata mazoezi na maarifa katika shughuli za kibiashara/kujifunza jinsi ya kuweka pamoja mawazo na mipango katika biashara yako
- Kupewa nasaha yako binafsi kabla ya kuanza biashara
- Kupewa nasaha binafsi kuhusu biashara iliyopo
- Mipango ya usaidizi kwa wanawake wenye uwezekano na ari kubwa katika biashara.
- Kuingia katika mtandao wa makundi ya wanawake wafanyao biashara
- Ukaguzi wa mifano bora

Tuna uratibu wa siku 12 juu ya kuanzisha biashara (kwa ajili ya wanawake walio na hati kamili ya ukimbizi Walio na Ulinzi wa Huduma za Kiutu au Ruhusa Maalum)

Uratibu huu utashughulikia:

- Kuongeza maarifa kama njia ya kujenga kujiamini, kutetea haki kuweka motisha
- Kuboresha ujuzi wako katika mawasiliano, kama msaada katika maisha na kazi yako
- Kujifunza kuzalisha mawazo yenye faida katika biashara yako
- Kujifunza jinsi ya kutayarisha mipango ya biashara yako
- Kuboresha ujuzi wako wa lugha ya kiingereza kwa manufaa ya maisha na biashara yako
- Upo msaada wa kifedha na msaada kwa ajili ya watoto na ya usafiri
- *Ili kupewa nafasi katika ratiba hii maalumu piga simu nambari: 02476 236 111*

Wasiliana nasi

Kwa kiwango chochote kile ulicho fikia katika mipango ya kibiashara au maendeleo ya kibiashara, tupo kwa ajili ya kukusaidia kuendeleza mawazo katika biashara yako, na kufanya ndoto zako kuwa kitendo halisi, kwa hiyo, tafadhali wasiliana nasi, kupitia afisizetu za Kijimbo kama ifuatavyo: (Jumaatatu hadi Ijumaa hadi saa 3 asubuhi hadi saa 11 unusu jioni) (9:00 until 17:30).

- Iwapo uko eneo la mjini au Jiji tafadhali piga simu 02476 236 111 (Women's Development Business Agency)
- Iwapo uko eneo la kijijini au soko mjini piga simu 01952 815 319 (Women in Rural Enterprise)

Iwapo hauna uhakika, wasiliana nasi, tuna kuhakikishia usaidizi. Waweza pia kuwasiliana nasi kupitia mtandao wa intaneti kwenye www.rweu.co.uk.

Tafadhali elewa kuwa

Iwapo unataka kukuza biashara yako kwa ufanisi nchini Uingereza, kudhibiti sawasawa lugha ya kiingereza ni muhimu

Idara za Mashirika yote ya kijimbo ya Wanawake Watendaji (Regional Women's Enterprise Unit) inachapisha vifaa vya mafunzo katika lugha ya kiingereza, utahitaji kuwa na kiwango cha ujuzi wa lugha ESOL kidatu cha 3 (tatu) (ESOL entry level 3).

Wafadhili wetu

RWEU hufadhiliwa kwa kiasi na:

